

## Maswali

1. Wake wawili wa Elkana waliiitwa nani?
2. Mbona Hana alikuwa na uchungu?
3. Hana alienda wapi?
4. Aliomba nini?
5. Aliahidi kwamba atamfanya Mungu nini ikiwa atampa mwana?
6. Hana aliita mwanawe eti nani?
7. Hana alipeleka Samweli kuishi wapi?
8. Usiku moja Samweli alidhani nani alikuwa anamwita?
9. Nani alikuwa akimwita?
10. Mungu aliyea Samweli ujumbe gani?

## Majibu

1. Hana na Penina.
2. Hana alikuwa na uchungu kwa sababu hakuwa na mtoto.
3. Hana alienda kwa Nyumba ya Mungu kuomba.
4. Hana aliomba apewe mtoto mvulana.
5. Aliahidi kwamba akipata mwana, atamtola Mungu huyo mtoto.
6. Hana alimwita yule mtoto Samweli.
7. Hana alimpeleka huyo mtoto kuishi Shilo kwa Nyumba ya Mungu.
8. Samweli alidhani kwamba Eli alikuwa akimwita.
9. Mungu alikuwa anamwita Samweli.
10. Mungu alimwambia Eli kwamba wanawe wawili watakufa. Eli naye atakufa. Samweli ndiye atakuwa kiongozi mpya.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



# 23 Mungu anamwita Samweli

## Marejeo

1 Samweli mlango wa1 na 3

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu alijibu maombi ya Hana ya imani na vile Samweli alikua kwa kumpenda Mungu na kumtumikia

## Maneno maalum

- 23.1 Elkana + wake 2 + Hana + hana watoto + Penina + watoto + karamu ya pasaka
- 23.2 Hana alikuwa na uchungu + Nyumba ya Mungu + omba + aliomba apewe mtoto mvulana + peana mtoto kwa Mungu + kuhani Eli + bariki Hana
- 23.3 Hana + mtoto mvulana + Samweli + akakua akawa mvulana + Nyumba ya Mungu + Eli + Samweli alimtumikia Mungu
- 23.4 Eli mzee + Samweli analala + sauti inaita + sio Eli + mara 3 Mungu akiita
- 23.5 Mungu + Samweli + wana wa Eli watakufa + Eli atakufa + Samweli kiongozi mpya

**23.1** Elkana alikuwa na wake wawili – Hana na Penina. Penina alikuwa na watoto kadhaa lakini Hana hukuwa nao. Elkana alipenda Hana sana. Kila mwaka Elkana na familia yake walienda Shilo kufanya Karamu ya Pasaka kukamilisha vile Mungu alitaka Wayahudi wote wafanye.

Kwa karamu Elkana alimpa Penina na watoto wake zawadi lakini alimpa Hana zawadi kubwa sana kwa sababu alimpenda zaidi. Penina alichokoza Hana tena alikuwa mbaya kwake eti kwa sababu hakuwa na mtoto. Hana alikuwa na huzuni sana kwa sababu alitaka mtoto sana.

**23.2** Mwaka fulani walipokuwa kwa Sherehe, Hana alikuwa na uchungu kabisa. Hakukula chakula chochote kwa Karamu ya Pasaka. Elkana alikuwa na wasiwasi juu ya Hana. Alimuuliza, “Ni nini mbaya? Mbona unalia? Tena mbona hauli chakula?” Lakini Hana kwa huzuni alitingisa kichwa chake tu.

Hana alienda kwa Nyumba ya Mungu kuomba. Kuhani alikuwa amekaa kwa hiyo Nyumba ya Mungu. Hana aliambia Mungu shida zake zote na hata vile alikuwa anataka mtoto. Aliuliza Mungu ampe mtoto mvulana. Aliahidi Mungu kwamba atampa huyo mtoto.

Hana alikuwa akiomba kwa nguvu na midomo tu ndiyo ilisogeza lakini sauti haikusikika. Eli alikuwa akimwangalia halafu akasirika kwa sababu alimdhania kwamba amelewa. Hana alimjibu kwamba alikuwa anaomba Mungu. Eli alimbariki na akauliza Mungu amwezeshehe alichotaka sana.

**23.3** Mwaka uliofwata Hana alipata mtoto mvulana mzuri. Alimwita yule mtoto Samweli, maana yake “Omba Mungu.” Hana alifurahi sana sana. Hakuenda Shilo tena mpaka Samweli alipokuwa mvulana mkubwa. Halafu akamvalisha nguo nzuri, akachukua ng’ombe wa kiume wadogo 3, unga na mafuta akapelekeea Eli kama zawadi kwa Mungu.

Hana alielezea Eli kwamba huyo ndie mtoto aliomba kwa Mungu. Alikuwa ameahidi kwamba atapea Mungu maisha yake yote. Kwa hivyo Hana alimwacha na Eli kwa Nyumba ya Mungu. Samweli aliishi kwa Nyumba ya Mungu na akamtumikia. Hana alikuja Shilo kila mwaka kwa Karamu ya Pasaka. Alimpelekea Samweli koti mpya na zawadi kila mwaka.

**23.4** Eli alikuwa mzee sana kwa hivyo Samweli alikuwa akimzaidia na kumwangalia. Usiku moja, Samweli alipokuwa amelala, aliamshwa na sauti ikimwita, “Samweli! Samweli!” Samweli alikimbia kwa Eli na kumuuliza, “Niko hapa, uliniita?”

Lakini Eli hakuwa amemwita. Kwa hivyo Samweli alirudi kulala. Alipokuwa anataka kulala, alisikia sauti tena, “Samweli! Samweli!” Samweli alirudi kwa Eli. Akamuuliza, “Niko hapa, uliniita?” Eli alimjibu, “Sikukuita mwanangu, rudi ulale.” Samweli alitatizika, lakini alirudi kulala.

Baada ya muda mchache alisikia sauti ikimwita tena, “Samweli! Samweli!” Mara tena Samweli alirudi kwa Eli. “Niko hapa, uliniita?” Papo hapo Eli akakundua kwamba lazima awe Mungu ndiye anaita Samweli. Aliambia Samweli, “Rudi ulale na ukisikia sauti tena sema, ‘Nena Bwana, kwa kuwa mtumishi wako anasikia.’”

Samweli alirudi kulala. Akasikia sauti inamwita, “Samweli! Samweli?” Alijibu, “Nena Bwana, mtumishi wako anasikia.”

**23.5** Mungu aliambia Samweli kwamba ataadhibu wana wa Eli wawili kwa sababu ni waovu. Alimwambia Samweli, hao wana wa Eli wawili watauawa hivi karibuni naye Eli atakufa pia. Samweli utakuwa kiongozi mpya utakayefundisha watu juu ya Mungu.

Asubuhi, Eli aliita Samweli na kumuuliza maneno yenye Mungu alikuwa amesema. Mwanzoni Samweli aliogopa kumwambia Eli lakini huyu kuhani mzee aliendelea kumuuliza, kwa hivyo Samweli alimwambia ukweli wa maneno yenye Mungu alisema. Eli akasema, “Ndiye Bwana, na afanye analoliona ni jema.”

